

1410/206  
KISWAHILI  
Juni/Julai 2019  
Muda: saa 3



THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL  
NATIONAL CERTIFICATE IN SOCIAL DEVELOPMENT

KISWAHILI

3 hours

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

*Mtihani huu una sehemu NNE muhimu:*

*insha, ufahamu, matumizi ya lugha na mbinu na vifaa vya kufundisha.*

*Jibu maswali yote kwenye kijitabu ulichopewa.*

*Ni muhimu sana ufuatae maagizo uliyopewa mwanzo wa kila sehemu.*

*Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

**Kijitabu hiki kina kurasa 5 zilizopigwa chapa.**

**Watahini ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi  
ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

**SEHEMU YA KWANZA: INSHA** (alama 20)*Jibu maswali yote katika sehemu hii.*

1. Andika insha isiyopungua kurasa mbili wala kuzidi kurasa mbili na nusu juu ya mojawapo ya vichwa vifuatavyo:
  - (a) Sinema za ughaibuni zina hasara nyingi. Jadili.
  - (b) Andika insha inayomalizia kwa:
 

..... Kijasho chembamaba kilianza kumtoka usoni huku akionyesha wasiwasi. Nilitambua wazi kuwa yeye ndiye aliyefanya kitendo hicho hasi!
  - (c) Akipenda chongo huita kengeza.
  - (d) Wewe in raia katika nchi ya Mzalendo. Mwandikie barua mhariri wa gazeti la Kumekucha Leo ukitoa maoni yako jinsi serikali yako inavyoweza kupunguza umaskini nchini.

**SEHEMU YA PILI: UFAHAMU** (alama 30)*Jibu maswali yote katika sehemu hii.*

2. Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Kutokana na nafasi yake katika harakati za ukombozi wa mataifa ya Afrika Mashariki hususan katika nchi ya Kenya na Tanganyika, kiswahili kiliibuka kuwa sehemu muhimu sana ya utamaduni wa mataifa hayo. Katika makala haya, tutaangazia jinsi kutokuwepo kwa sera madhubuti katika sekta ya elimu nchini Kenya kulivyochelewesha kukuwa na kuenea kwa Kiswahili. Baada ya uhuru, sera ya lugha nchini Kenya imekuwa ikiongozwa na mapendekezo ya tume mbali mbali zilizoteuliwa kuchunguza masuala yanayohusu Kiswahili. Kati ya tume sita zilizoundwa ili kuchunguza matumizi ya lugha shuleni, ni timu ya Mackay tu iliyotoa mapendekezo muhimu yaliyoishia kukifanya Kiswahili somo la lazima na la kutahiniwa katika shule za msingi na za upili.

Tume ya Ominde iliyoteuliwa mwaka wa 1964, haikuona umuhimu wa kukifanya Kiswahili somo la lazima shuleni. Mapendekezo yaliyotolewa na tume yenyewe hayakuwa na mchango mkubwa katika kukua na kuenea kwa Kiswahili. Kwanza ilipendekeza kufunzwa kwa Kiswahili shuleni bila kutahiniwa. Pili, ilipendekeza kuendeshwa kwa mafunzo ya Kiswahili kwa walimu wa shule za msingi wakati wa likizo. Mapendekezo haya mawili yanaonyesha jinsi tume yenyewe ilivyopuuza umuhimu wa lugha ya Kiswahili. Kimsingi, iwapo somo linafunzwa



shuleni bila kutahiniwa, halitakuwa na athari kubwa kwa wanaofundishwa. Matumizi mabaya ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanasiasa wakongwe waliosoma wakati huu ambapo Kiswahili hakikupewa nafasi muhimu katika mfumo wa elimu yamkini ni matokeo ya sera hiyo ya kuyumbayumba.

Tume ya Wamalwa ilyofuata ile ya Ominde na iliyoanzishwa mwaka wa 1972 nayo haikuwa na mchango mkubwa katika kukuza na kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Tume hiyo iliweka msisitizo katika ufundishaji wa lugha za kimataifa kama vile Kifaransa na Kijerumani shuleni. Tume ya Wamalwa ilipendekeza Kiswahili kitumiwe katika kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma wakiwamo wakuu wa wilaya ambao hawakuweza kuwasiliana vyema kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Pendekezo lenyewe lilikuwa sawa sawa na kuukunja mti ambao tayari ulikuwa umekomaa. Njia mwafaka zaidi ambayo ingesaidia kuipiga msasa lugha ya watumishi wa umma ingalikuwa kuweka msingi madhubuti wa lugha ya Kiswahili katika mfumo wa elimu.

### MASWALI

- (a) Ipe taarifa hii kichwa kifaacho. (alama 2)
- (b) Taja tume tatu zilizotajwa katika makala haya. (alama 3)
- (c) Kwa kila tume uliyotaja toa mapendekezo mawili yaliyotolewa. (alama 6)
- (d) Ni nini hasa kilichangia kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya? (alama 2)
- (e) Ingawa kumeteuliwa tume mbalimbali za kushughulikia swala la sera ya lugha nchini Kenya, bado hakuna sera mwafaka. Eleza sababu nne. (alama 8)
- (f) Taja lugha zozote tatu ambazo ni za kimataifa. (alama 3)
- (g) Toa maana ya msamiati ufustao kama ulivyotumika katika taarifa: (alama 6)
- (i) sera madhubuti;
  - (ii) kuyumbayumba;
  - (iii) mapendekezo;
  - (iv) mfumo wa elimu;
  - (v) tume ya uchunguzi;
  - (vi) kuukunja mti ambao tayari umekauka.

(j) Eleza maana ya methali hii:

Ukiona vyaelea jua vimeundwa.

(alama 2)

**SEHEMU YA NNE: MBINU ZA KUFUNDISHIA** (alama 20)

*Jibu mwaswali yote katika sehemu hii.*

4. (a) Wewe kama afisa anayesimamia maswala ya jamii katika kaunti ndogo yako, umcalikwa na vikundi vya vijana ili kuwaelekeza jinsi wanavyoweza kuandaa tamasha za michezo mbalimbali. Eleza mbinu mbalimbali utakazotumia. (alama 10)
- (b) Andika hadithi fupi inayotoa funzo kwa vijana kuhusu madhara ya ugonjwa wa ukimwi. (alama 10)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**